PONGEZI>> Baraza laridhishwa kukamilika kwa ujenzi wa Chuo

# Neema tupu usafirishaji nyama ya mbuzi, kondoo

ASHURA ASSAD Na REHEMA MAIGALA

USAFIRISHAJI wa shehena ya mbuzi na kondoo, umeshika kasi baada ya Bodi ya Nyama Nchini, kusema wameanza tena kufanya hivyo ikiwa ni utekelezaji wa mkakati wa kuongeza mapato kupitia sekta ya mifugo.

Awali, usafirishaji huo ulikuwa wa kusuasua kutokana na changamoto zilizokuwepo, ikiwemo uhaba wa viwanda na teknolojia.

Imesema kwa sasa wanasafirisha kwenda nje ya nchi zaidi ya tani 60,000 kwa wiki ambapo masoko yake ni Kuwait, Qatar na Hong Kong.

Usafirishaji huo umetokana na kuongezeka kwa ubora wa nyama ya Tanzania, uliochangiwa na ufugaji bora na kisasa wenye kufuata vigezo na masharti ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili hivi karibuni, Kaimu Msajili wa bodi hiyo, Imani Sichwale, alisema usafirishaji wa nyama hizo ulianza Agosti 12, mwaka jana.

Sichwale alisema hali iliyopo sasa, kwa wiki moja wanasafirisha mbuzi na kondoo 61,540 wakiwa wameshachakatwa na kuwa nyama.

Kwa mujibu wa Kaimu Msajili huyo, uchakataji wa nyama una faida kubwa kwa nchi ikiwemo ajira kwa wananchi na fedha za kigeni.

"Tumeamua kuchakata nyama hii kwa sababu ya uwepo wa viwanda nchini na kudumisha uzalendo kwa wazawa kwa kuwapatia ajira inayotokana na mifugo yetu.

"Kama tungesafirisha wanyama wakiwa wazima, tungepeleka ajira zetu nje ya nchi na kuwaacha Watanzania wakiendelea kulilia ugumu wa ajira nchini," alisema.

Alisema kutokana na changamoto mbalimbali ambazo hazijapatiwa ufumbuzi, wanalazimika kusafirisha shehena za nyama kwa njia ya anga kwa wiki, si kila siku.

Hata hivyo, alisema anaamini changamoto mbalimbali zilizopo zitaendelea kutatuliwa kwa wakati, kwa kuwa ni moja ya ahadi zilizomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Alisema usafirishaji huo wa nyama kwenda nje ya nchi sasa utakuwa endelevu na serikali imejipanga kuongeza soko la bidhaa hiyo nje ya nchi ambazo zinafikiwa sasa.

"Moja ya changamoto ni upatikanaji wa vibali vya usafirishaji bidhaa hiyo hivyo bodi imeamua kukutana na wizara husika ili kutatua changamoto hiyo kwa lengo la kukuza soko la ndani na nje," alisema.

Akizungumzia upatikanaji wa mifugo inayochakatwa na kukusanywa kutoka kwa wafugaji mbalimbali na taasisi za kiserikali ambazo zimesajiliwa, alisema wafugaji hawatafuti masoko, isipokuwa bodi ndiyo inamjulisha mfugaji kwa ajili ya kupeleka mifugo iweze kuchakatwa na kusafirishwa.

HALI ILIVYOKUWA AWALI

Sichwale alisema awali usafirishaji wa nyama nje ya nchi, ulikuwa wa kusuasua, kutokana na changamoto zilizokuwepo, ikiwemo uhaba wa viwanda na teknolojia.

Alisema hivi sasa kasi ya kusafirisha nyama kwenda nje ya nchi imeongezeka, ambapo kwa wiki kiwanda cha Tan Choice kilichopo Kibaha, Pwani, kinasafirisha nyama kilo 60,000 sawa na tani 60 kwenda Oman, Qatar na Kuwait.

Kwa mujibu wa Sichwale, katika mwaka wa fedha 2017/208, wasitisha huduma za usafirishaji wa nyama kwenda nje ya nchi.

Alieleza mwaka uliofuata wa fedha 2019/2020, walirejea kusafirisha nyama hizo ambapo walikuwa wakisafirisha zaidi ya tani 692.46 ambazo ni sawa na kilo 69,200.

"Kwa kipindi hicho, kwa wiki moja, viwanda vilivyokuwepo vilikuwa vinasafirisha nje ya nchi nyama tani 8.84 sawa na kilo 8,840 tu," alisema.

Alisema kiwanda cha Eliya Foods Overseas Limited, hivi karibuni kilianza kupeleka nyama katika soko jipya la Hong kong.

"Kiwanda hiki kimeanza kupeleka nyama ya mbuzi kwenda Oman, ambayo inafika uzito wa kilo 1,874 sawa na tani 14.6," alisema Sichwale.

AHAMASISHA UFUGAJI BORA

Sichwale aliwataka wafugaji kuhakikisha wanazingatia ufugaji wa kisasa ili mifugo yao iwe na ubora unaostahili.

Akizungumzia usalama wa nyama wanaangalia isiwe na wadudu waharibifu isilete magonjwa na isiyoharibika kwa haraka, alisema wataalamu wa nyama waliosomea wamekuwa wakijua usalama wa mnyama kwa ajili ya matumizi ya binadamu, hivyo aliwashauri kuwatumia hao kabla ya kumchinja mnyama.

WASOMI WAPONGEZA

Baadhi ya wasomi wamepongeza usafirishaji huo wa nyama kwenda nje ya nchi, kwani utaongeza tija kwa Taifa na kipato cha wafugaji.

Mhadhiri wa Uchumi kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Dk. Timothy Lyanga, alisema usafirishaji wa nyama tani 60,000 unaonesha dhahiri dhamira ya serikali kwamba inatumia mbinu mbalimbali kwa ajili ya kupata fedha za kigeni lengo likiwa ni kuliongezea pato Taifa.

Dk. Lyanga alisema kinachotakiwa kufanyika kwa sasa ni kufuga mifugo iliyo bora na kwa njia ya kisasa ili kukidhi mahitaji ya soko la kimataifa.

Pia, alisema wafugaji wanatakiwa kuelimishwa zaidi ili wafuge mifugo iliyo bora kwa ajili ya kuuza bei na kuwaletea manufaa.

"Serikali imeshatoa njia nzuri kwa wafugaji kinachotakiwa hivi sasa ni kufuga mifugo iliyo bora kwa njia ya kisasa ili kujiongezea kipato kikubwa," alisema.

Naye, Mhadhiri wa Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha MaryLand cha Marekani, Dk. Josephat Warema, alisema usafirishaji wa bidhaa ya nyama kwenda nje ya nchi ni faida kubwa kwa wafugaji kwa kuwa wamepata soko la uhakika.

Dk. Warema alisema si kwa wafugaji pekee yao, hata Taifa litajiongezea uchumi kutosha katika usafirishaji wa bidhaa hiyo.

Hata hivyo, alisema Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa wingi wa mifugo Afrika, hivyo nafasi iliyopatikana itasaidia kuboresha mifugo hiyo kuwa ya kisasa na bora zaidi.

"Tuache kufuga kienyeji, tufuge kisasa, ili kujiongezea tija na kipato katika taifa na kwa wafugaji," alisema.

WANANCHI WAPONGEZA

Baadhi ya wananchi waliozungumzia hatua ya Tanzania kuanza kusafirisha shehena ya nyama kwenda nje ya nchi, walisema ni turufu nyingine inayokwenda kutanua fursa za kiuchumi kwa nchi.

Mkazi wa Majohe, Jacob Daniel, alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na mifugo mingi, hivyo kupatikana kwa masoko nje ya nchi, kutachochea ufugaji na kuongeza ajira.

"Nawapongeza waliofanikisha upatikanaji wa masoko hayo, naamini tutasikia mabilioni mengine yakiingia katika nchi kutokana na mifugo ambayo sasa itakuwa turufu ya maendeleo ya kiuchumi," alisema.

Naye, Mkazi wa Sirari Mkoani Mara, Baraka Oluwochi, aliiomba serikali itanue fursa ya ukusanyaji mifugo hiyo inayochakatwa na kusafirishwa nyama ili hata wafugaji walioko maeneo ya pembezoni mwa nchi wanufaike.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kwa mwaka 2020-2025, imetaja mpango wa serikali wa kununua ndege mpya tano, ikiwemo moja ya mizigo.

Hatua hiyo inatajwa kuwa sababu nyingine itakayohamasisha ukuaji wa sekta ya mifugo na uvuvi nchini, hasa ikizingatiwa kuwa ndege hiyo inatarajiwa kuwa na mifumo ya majokofu ya kuhifadhi minofu ya nyama na mbaogamboga.

UHURU UK 5.

# Fursa zazidi kumiminika uuzaji samaki nje ya nchi

Na REHEMA MAIGALA

KAMPUNI nane za Kitanzania, zimepewa kibali cha kuingiza na kusambaza samaki katika nchi ya Saudi Arabia ikiwa ni matokeo ya mikutano ya kibiashara iliyofanyika kwa njia ya kimitandao.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ali Mwadini, wakati akizungumza na wazalishaji wa bidhaa za kilimo, Ufugaji na Uvuvi, jijini Dar es Salaam.

Balozi Mwadini alisema kibali hicho kimetolewa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya nchini humo (SFDA), baada ya kampuni hizo kukidhi taratibu za nchi zote mbili na kuridhiana kuingizwa kwa bidhaa hiyo.

Alisema kwa sasa wanashughulikia kibali kingine cha kuingiza bidhaa ya asali nchini Saudi Arabia kwa kuwa ni bidhaa ya chakula inayohitajika kuchakatwa kwanza kabla ya kuuzwa katika nchi hiyo.

"Nawaomba wazalishaji wa bidhaa ya asali wawasilishe taarifa zao katika Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) ili zifanyiwe taratibu za kuombewa vibali,"alisema.

Balozi Mwadini alisema licha ya kushughulikia kibali cha asali na samaki pia wapo katika mpango wa kupata kibali cha kuingiza nyama nchini Saudi Arabia.

"Kwa wanaofanya biashara ya nyama lazima wakidhi vigezo vya kuwa na cheti halali pamoja machinjio yaliyothibitishwa na mamlaka zinazohusika na usimamizi wa nyama nchini ili kuweza kuingiza nyama safi nchini Saudi Arabia,"alisema

Alisema kampuni za Serikali na binafsi nchini Saudi Arabia zinazohusika na uwekezaji wa sekta ya kilimo na mifugo ambao wanahitaji wabia wa kuzalisha bidhaa nchini mwao ili wapeleke.

"Wanahitaji kuanzisha shamba la mifugo na machinjio yatakayoweza kuchinja vichwa 4000 vya mbuzi kwa siku na kondoo, hivyo ikiwa kuna Mtanzania anayehitaji kuwa mbia ubalozi upo tayari kushirikiana katika kufanikisha hili," alisema .

Alisema pia kuna fursa ya upatikanaji wa mtaji wa vitendea kazi katika uzalishaji wa bidhaa, hivyo kama kuna Mtanzania mwenye mradi wa kilimo na uhitaji wa vifaa vya kilimo kuna makampuni yako tayari kuwapatia vifaa vya kilimo.

Balozi Mwadini alisema bidhaa asilimia kubwa ya bidhaa zinazoingizwa nchini humo ni chakula kwa sababu nchi hiyo ni jangwa na uchumi wake utegemea mafuta.

Hata hivyo, Balozi Mwadini aliwaondoa hofu wafanyabiashara na kuwahakikishia soko la uhakika na kuwataka kugeuza changamoto za ndani kuwa fursa kwenye eneo la uzalishaji, ufungashaji na utunzaji bora wa bidhaa ili kuweza kupenya katika soko hilo.

Scanned with CamScanner

ti huo
ha ud-
aya ya
kosefu
wa ka-
nzi za

i kuto-
ko na
mwa-
isavyo
o kwa

# SMZ: Uvuvi maeneo yaliyotengwa endelevu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu, imesema doria za uvuvi katika maeneo ya hifadhi yaliyotengwa na serikali ni endelevu kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu na rasilimali za baharini.

Hayo yalisemwa na Waziri wa wizara hiyo, Abdalla Hussein Kombo, wakati akitoa ufafanuzi na kujibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu, Haji Omar Kheir, aliyetaka kujua kwa nini wavuvi wanasumbuliwa wakati wanapofanya shughuli za uvuvi katika kisiwa cha Tumbatu.

Kombo alisema si kweli wavuvi wanasumbuliwa wakati wakifanya shughuli za uvuvi cha msingi wafuate sheria za uvuvi zilizopo.

Alieleza imebainika wapo wavuvi wanaendesha uvuvi katika maeneo ya hifadhi tengefu, ambayo yametengwa kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu.

Alisema kisiwa cha Tumbatu ni moja ya eneo tengefu lililopo katika hifadhi ya kitaifa na kuona rasilimali za uvuvi wa baharini zinalindwa.

"Mheshimiwa Spika, wapo wavuvi wanajipenyeza na kuendesha uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi ambayo yametengwa kwa ajili ya kulinda rasilimali za baharini," alisema Kombo.

Aliwataka wavuvi kuhakikisha wanafuata taratibu na sheria mbalimbali za kulinda rasilimali ya uvuvi wa baharini na kuacha kutumia mitego ambayo imepigwa marufuku na idara ya maendeleo ya uvuvi.

"Ipo sheria 11 ya Uvuvi ya Mwaka 2015 imepiga marufuku aina ya uvuvi ikiwamo wa kutumia mishale ambao unatishia uharibifu wa mazingira ya matumbawe ambayo ndiyo mazalia ya samaki na viumbe vya baharini," alisema.

MWANANCHI UK 24.

# * Bei ya dagaa yapaa *

Saada Amir, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Mwanza.** Baadhi ya wakazi wa jiji la Mwanza wamegeukia dagaa wa chukuchuku baada ya wafanyabiashara wa kitoweo hicho kupunguza vipimo vya dagaa wa kukaanga na wengine kupandisha bei.

Kwasasa kipimo cha dagaa waliokaangwa kilichokuwa kinaunzwa Sh500 kinagawanywa mara mbili ili kufidia gharama za mafuta ya kula huku baadhi ya wafanyabiashara wakipandisha bei kutoka Sh500 kufikia Sh1,000.

Jijini Mwanza, lita tano ya mafuta ya kula inauzwa Sh28,000, lita 10 ni Sh43,500 na lita 20 ikiuzwa Sh81000.

Akizungumza gazeti hili, mfanyabiashara Monica Lawrence alisema kwa sasa wananunua lita tano ya mafuta ya kula kwa Sh28,000 na imewalazimu wapunguze kipimo na wengine wamepandisha bei. Mkazi wa Mtaa wa Mlungushi Kata ya Igogo jijini Mwanza Pendo Daniel alisema watu wenye familia kubwa hulazimika kununua dagaa wabichi na kuwaunga kwa nyanya.

Scanned with CamScanner

# Watakiwa kuondoa watoto kambi za uvuvi

**Mwenyekiti wa kambi ya uvuvi ya Migongo, Masau Malegesi alisema changamoto ya watoto kuishi kwenye kambi hizo zinatokana na wanaume kutekelekeza familia zao, hivyo wanawake kulazimika kwenda na watoto kwenye kambi hizo.**

**Daniel Makaka**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Sengerema.** Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole ameagiza viongozi wa kambi za uvuvi kuhakikisha watoto wenye umri chini ya miaka 18 walioko kwenye kambi hizo wanaondolewa ndani ya siku 14.

Kipole alitoa agizo hilo jana alipozungumuza na *Mwananchi* na kueleza kukerwa na hali hiyo.

Tangu mwaka 2018 kumekuwa na ongezeko la watoto kwenye kambi za uvuvi ya Kome mchangani, Kabiga, Migongo, Lulagazi kubwa, Bugombe pamoja na Lubalazi ndogo wakifanya kazi ya kuuza matunda, kusomba samaki na kusomba maji kwa ajili ya nyumba za wageni.

"Maeneo hayo yote ni hifadhi, hivyo kwa mujibu wa sheria watoto wote mwenye umri chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kuishi kwenye maeneo hayo, hivyo wanatakiwa kuondoka waende shule," alisema Kipole.

Mhifadhi wa misitu wilaya ya Sengerema, James Alyoce alisema alishatoa tamko kwa wavuvi wakae hifadhini na kufanya shughuli zao bila watoto hasa ambao wamefikisha umri wa kwenda shule.

Alyoce alisema jukumu la kuwakamata wavuvi wanaoishi na watoto maeneo yao wanayofanyia kazi na kusababisha wasiende shule si jukumu lao, bali ni la uongozi wa kata na vijiji husika kwa kushirikiana na na idara ya elimu.



DODOMA N

From DAILY NEWS Reporters in Dodoma

# Over 2bn/- allocated to fight ocean, lake crime

THE government has launched a 2.07bn/- ($900,000) programme to combat crime in the Indian Ocean and lakes.

The programme, jointly funded by Japan and UNDP, was launched at the weekend

Japan has injected over 1.1bn/-. ($500,000) into the project and UNDP covers the remaining amount.

Speaking during the launch, Permanent Secretary in the Prime Minister's Office (Policy and Coordination) Dorothy Mwaluko wanted institutions responsible for project implementation to ensure there is transparency, efficiency and diligence to meet the target.

"The executive committee which oversees the project has issued the terms of references, including a work plan, financial aspects and procurement details. All guidelines must be guided by professionalism during implementation," she insisted.

She said the government and other stakeholders expected changes by December this year.

She said with a modern security system, they expected to increase productivity.

"We would like to see the fisheries sector changing and improving. We need more storage facilities and use of modern fishing gear," she said.

According to Ms Mwaluko, the project is designed for implementation in the Indian Ocean from Tanga to Mtwara.

She said the government's intention was to control illegal fishing and other related crimes.

She asked members of the public, who resided along project areas to ensure they supported the government by protecting resources in their areas.

For his part, Permanent Secretary in the Ministry of Livestock and Fisheries, Dr Rashid Tamatamah, said the project would help the government end illegal fishing in the deep sea.

He said the deep sea fishing authority would improve its daily operations by empowering those who engaged in fishing by using sustainable fishing plans and by using vessels to protect marine resources.

UNDP Representative Christine Musisi said the government's focus on blue economy strategy was one of the indicators for the government's intention to improve people's welfare.

Project Coordinator Hassan Mrisho Kheri said they would deal with illegal fishing, drug trafficking and human trafficking which had been reported to be going on in deep sea.

Scanned with CamScanner

VII examinations, hence great efforts were needed to rectify the situation.

the construction of 500-metre bridge on Pangani river to connect with Bweni.

centres, beginning with two will ensure medicines will be available at all times.

THE GUARDIAN page 6.



**Hester livestock vaccination factory manager Dr Umapati Dasgupta (R) briefs Livestock and Fisheries ministry permanent secretary Prof Elisante ole Gabriel (L) during the latter's visit to the facility at Kibaha in Coast Region at the weekend.** Photo: Guardian Correspondent

Scanned with CamScanner